MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Nyimbo za Kiswahili kama mkakati wa kuhamasisha umma kuhusu UVIKO-19 nchini Kenya

Jamila Masitsa*, Kenneth Simala

*Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi, Shule ya Elimu, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kakamega, Kenya*

**IKISIRI**

Makala hii inajadili namna nyimbo zilivyotumika katika redio kuhamasisha umma kuhusu Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO-19). UVIKO-19 ni janga la kiafya la kimataifa ambalo lilivuruga maisha ya binadamu kote ulimwenguni. Kutokana na tishio la UVIKO-19, serikali na asasi mbalimbali zilijitolea kukabiliana na janga hili kwa kutumia mikakati tofauti tofauti ikiwemo kuhamasisha umma. Mkakati mojawapo ambao serikali ilitumia kuleta ufahamu dhidi ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona ulikuwa kutumia nyimbo za Kiswahili katika vyombo vya habari hasa redio ikichukuliwa kuwa dhima ya redio ni: kuburudisha, kuelimisha na kufahamisha. Makala hii inaonyesha namna ambavyo nyimbo hasa za kiswahili zilitumika katika redio kuhamasisha umma dhidi ya vipengele via mawasiliano ya kiafya kuhusu UVIKO-19. Inaonyesha jinsi nyimbo za Kiswahili zilivyosaidia uelimishaji na uhamasishaji wa umma dhidi ya UVIKO-19 na kuchangia pakubwa kubadili mawazo ya wananchi wa Kenya kwa njia ya burudani.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Nyimbo,
Uviko-19,
Uhamasishaji umma

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 06 Juni 2024
Tarehe ya Kurekebishwa: 30 Julai 2024
Tarehe ya Kukubalika: 10 Oktoba 2024
Mtandaoni: 27 Novemba 2024

## 1. Utangulizi

Janga la UVIKO-19 liliibuka na kuenea kote duniani na likawa tishio katika ulimwengu mzima. Lilikuwa suala la afya tangu Machi, 2020 na Zaidi ya watu milioni thelathini walipatikana kuambukizwa ulimwenguni (Lisco na wenzake, 2021). Ugonjwa huu ulisababisha vifo zaidi ya milioni 2.5 vya watu kufikia mwanzoni mwa 2021. Hali ya UVIKO-19 ilivuruga familia na jamii kutatizika.

Jed. 1 linaonyesha kuwa visa vya virusi vya korona nchini Kenya vilivyothibitishwa vilikuwa 323,160. Ulimwenguni kote, karibu visa vipya milioni 5.3 na vifo zaidi ya 48,000 viliripotiwa katika siku 28 (23 Januari hadi 19 Februari 2023), kupungua kwa 89% na 62%, mtawaliwa, ikilinganishwa na siku 28 zilizopita. Kufikia 19 Februari 2023, zaidi ya kesi milioni 757 zilizothibitishwa na zaidi ya vifo milioni 6.8 vimeripotiwa ulimwenguni, (WHO, 2023). Kufuatia jaribio hilo lililothibitishwa, serikali ya Kenya iliendelea kuchochea mfululizo wa mikakati ya kupunguza hatari ya visa kutoka nje na kuenea kwa virusi hivyo. Vizuizi vya usafiri viliwekwa, mikutano ikapigwa marufuku miongoni mwa masharti mengine.

Mnamo Machi 15, serikali ilianzisha hatua ambazo hazijawahi kushuhudiwa kudhibiti virusi; shule zote na taasisi za elimu ya juu zilifungwa, amri ya kutotoka nje kutoka saa 7 jioni hadi 5 asubuhi, wafanyikazi wa serikali na wa mashirika ya biashara walishauriwa kuanza kufanya kazi nyumbani; isipokuwa huduma muhimu, serikali pia ilisisitiza haja ya kufanya miamala isiyo na fedha taslimu na malipo ya kielektroniki ili kuzuia kuenea kwa virusi hivyo (WHO, 2020). Serikali iliongeza hatua zake kwa kuzuia mikusanyiko ya watu, kufutwa kwa sherehe na taasisi zote pamoja na tasnia ya usafirishaji zilitakiwa kufuata hatua kali za afya ya umma kama vile kusafisha, kuua vijidudu mara kwa mara, na kufanya mazoezi ya umbali wa kijamii ili kudhibiti kuenea kwa virusi. Serikali pia ilitangaza safu ya hatua za kuwaepusha walio hatarini kutokana na janga hili (Benki ya Dunia, 2020).

Ni kutokana na hali hii ambapo makala hii inajadili nafasi ya nyimbo za kiswahili kwenye kwenye redio ya kitaifa ya KBC (Kenya Broadcasting corporation), redio Citizen, redio Maisha na redio Jambo katika kuhamasisha umma kuhusu UVIKO-19 nchini Kenya.

### 1.1. Misingi ya Nadharia

Makala hii inaongozwa na kiunzi cha nadharia kilichojikita kwenye nadharia mbili kuu: Nadharia ya Mawasiliano ya Kiafya (Thompson & Schulz, 2021) na

* Mwandishi Mkuu. Simu: +254715676684; Barua Pepe: jamilamasitsa@gmail.com

Mhariri: Pamela Ngugi, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Nukuu: Jamila M., & Kenneth S. (2024). Nyimbo za Kiswahili kama mkakati wa kuhamasisha umma kuhusu UVIKO-19 nchini Kenya. Jarida la Kiswahili Sanifu 1(2024), 26 – 32.

© 2024 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

Nadharia ya Eliburudani (Zorica, 2014). Nadharia hizi mbili ziliteuliwa kwa sababu zinachangiana na kukamilishana katika kushughulikia suala la UVIKO-19. Nadharia ya mawasiliano ya kiafya inasisitiza mambo ya kimsingi yafuatayo; Kwanza, utambuzi wa suala la kiafya linalohusika; Pili, uzingatiaji wa muktadha ambamo suala la kiafya linatokea; Tatu, aina za mawasiliano muafaka kuhusu suala la kiafya; Nne, jukwaa la mawasiliano ya kiafya; Tano, mpangilio wa mawasiliano; Sita, maandalizi na matumizi ya ujumbe wa kiafya; na Saba, athari ya ujumbe wa kiafya kwa wale waliolengwa. Kwa upande mwingine, nadharia ya Eliburudani imetumika kwa mujibu wa Zorica (2014). Kulingana na Zorica (2014), nadharia ya Eliburudani hufinyanga dhana mbili kwa pamoja: matumizi ya vipengele vya burudani katika elimu, na uhusishaji wa masuala ya kielimu katika burudani. Lengo kuu la kuseta masuala haya ni kufanikisha ujifunzaji kupitia burudani kwa minajili ya kubadilisha tabia. Nadharia ya mawasiliano ya kiafya ilitumika katika kuchanganua namna nyimbo za Kiswahili zilitumika kwenye redio nchini Kenya zilivyochangia kukabiliana na UVIKO-19. Makala hii imechambua ujumbe kuhusu UVIKO-19 katika nyimbo za Kiswahili kwenye redio teule na namna unavyoilenga umma kwa kuihamasisha. Vilevile, makala hii ilionyesha redio kama jukwaa linalotumika kuwasilisha ujumbe kwa umma kuhusu UVIKO-19. Isitoshe, utafiti ulitathmini namna ambavyo ujumbe, lugha na redio vinavyoshirikiana kuhakikisha kwamba umma inabadili tabia na mienendo ya kukabiliana na UVIKO-19.

**Jed. 1: Ripoti ya Visa vya UVIKO-19**

| Tarehe | Visa vilivyothibitishwa | Vifo |
|---|---|---|
| 11 Machi 2022 | 323,160 | 5,644 |
| Novemba 2022 | 340,431 | 5,680 |
| 23 Januari- februari 2023 | 5,300,000 | 48,000 |
| 19 Februari 2023 | 757,000,000 | 6,800,000 |

## 1.2. Uhakiki wa Maandishi

Hatari na tishio la UVIKO-19 ni masuala yaliyosababisha umuhimu wa uhamasishaji wa umma kuhusu janga hili kuwa mambo ya dharura. Athari ya UVIKO-19 kama vile maambukizi na vifo, sababu na njia za kuenea, na mbinu za kukabiliana na ugonjwa ni mambo ambayo umma inahitaji kuyafahamu (Mackay na Arden, 2015; Rabbani & Mahtab, 2020). Utafiti wa Momattin na wenzake (2013) uliofanywa kuhusu aina ya UVIKO-19 ya hapo awali ulionyesha kuwa umma ikihamasishwa huelewa na kuchukua hatua za tahadhari na hivyo kupunguza tishio la ugonjwa. Uhamasishaji husaidia umma kufanya uamuzi na kuchukua hatua za kupunguza kusambaa kwa UVIKO-19 (Jin, 2020). Mbali na hayo, uhamasishaji husaidia kutambua kwa haraka visa vya UVIKO-19 na kuchukua hatua muafaka.

Uhamasishaji ni mchakato wa kimawasiliano ambao hushirikisha umma katika suala fulani kwa ajili ya kubadili mielekeo, tabia na imani kulihusu jambo husika (Sayers, 2006). Uhamasishaji umetambulika na kuendelezwa kutokana na umuhimu wake wa kuleta mabadiliko katika jamii. Shirika la (UNEP, 2006) linadai kuwa umma ambayo imehamasishwa huwa hakikisho na kinga dhidi ya janga lolote katika jamii. Uhamasishaji wa UVIKO-19 ni ufahamu, mielekeo na tabia za umma kuhusu ugonjwa huu (Abuya na wenzake, 2020; Mahato & Suryavanshi, 2020). Kenya, kama nchi zingine duniani, ilikumbwa na janga la UVIKO-19 ambalo lilisababisha maafa kwa wananchi. Ni kutokana na hali hii ambapo uhamasishaji wa umma ni muhimu.

Uhamasishaji ni muhimu na unahitaji mkakati pia uhamasishaji wowote ule hulenga kuhakikisha ufanisi kuhusiana na jambo fulani kwa kuweka wazi suala husika kupitia uwasilishaji wa ujumbe. Matokeo ya uhamasishaji ni kubadili tabia na kuimarisha hali. Ufahamu ulioimarishwa wa umma ni muhimu katika kukabiliana na matatizo ya afya ya wakati wa milipuko. Kuwa na ujuzi wa kutosha wakati wa ugonjwa husaidia kuzuia na hatimaye kulinda afya (Brug na wenzake, 2004; Sadique na wenzake, 2007; Yıldırım na wenzake, 2020). Uhamasishaji huongeza ushirika wa kikamilifu katika mifumo ya kinga kuhusiana na kuenea kwa janga hili (Shafiq na wenzake, 2021). Kutumia njia mbalimbali za habari kama vile redio, magazeti, televisheni na maafisa wa serikali kwa ufanisi ni muhimu katika kuongeza ufahamu wa umma kuhusu maambukizi na matokeo yake (Van der Weerd na wenzake, 2011). Kazi hii itasaidia kuelewa umuhimu wa kuhamasisha umma dhidi ya UVIKO-19 kupitia nyimbo za kiswahili katika redio teule nchini Kenya.

Uhamasishaji wa umma hutegemea mawasiliano (Sayers, 2006) nayo mawasiliano hutokea kwa lugha ya maandishi, simulizi au taswira kama vile picha na mchoro. O'Sullivan (1983) anafafanua kwamba mawasiliano ni mchakato wa watu kutangamana na kubadilishana maana kuhusu jambo fulani kupitia ujumbe unaotokea katika mazingira na utamaduni. Mchakato huo hutokea kwa hatua tatu: uwasilishaji; upokeaji; na upatikanaji wa maana. Hatua hizi za kimawasiliano zinaweza kuathiriwa na chombo kinachotumika kuwasilisha ujumbe; uzoefu na maoni ya washiriki; na mazingira ya mawasiliano yanayoweza kuathiri maana iliyokusudiwa. Uhamasishaji mzuri unahitaji kuzingatia ujumbe mmoja pekee, au aina mbalimbali za ujumbe zinazohusiana, lakini siyo zaidi ya tano (Sayers, 2006). Mbali na ujumbe, uhamasishaji unafaa kutilia maanani hadhira inayolengwa ili kuandaa mkakati wa kimawasiliano, na kufahamu wakati wa kuwasiliana.

Makala hii ilichunguza namna mawasiliano ya kiafya yanavyojitokeza katika nyimbo za Kiswahili kwenye redio teule kwa ajili ya uhamasishaji wa umma nchini Kenya kuhusu UVIKO-19. Makala hii ilizingatia nyimbo za Kiswahili na kuchunguza iwapo zinaeleza lengo kupitia ujumbe na kwa kuzingatia hadhira. Ujumbe umehakikiwa ili kuelewa maana inayokusudiwa bila kuzua utata. Vile vile, ujumbe ulichunguzwa ili kuelewa kama unatumia lugha muafaka, sahili na nyepesi, inayoeleweka kwa haraka, kwa uwazi na kupitia njia mbalimbali.

## 2. Mbinu za Utafiti

Utafiti ulilenga nyimbo kuhusu UVIKO-19 katika redio ya Taifa ya KBC; redio Citizen; redio Maisha na stesheni ya redio Jambo katika uhamasishaji. Sampuli ya kimaksudi ilitumika kuteua nyimbo na stesheni zilizohusishwa. Nyimbo nne za Kiswahili zilizohusu UVIKO-19 ziliteuliwa kimaksudi. Nyimbo hizi ni: Korona, Korona hatari, Corona Virus Song (Wimbo wa Virusi vya korona) na gonjwa hatari. Njia za ukusanyaji data zilijumuisha usikilizaji, unukuzi, uratibu, usomaji wa kina na kisha uhifadhi. Kwanza, usikilizaji ambapo nyimbo za Kiswahili kwenye redio teule zilisikilizwa na kisha kurekodiwa. Pili, uratibu wa nyimbo za Kiswahili kwenye redio teule na uainishaji wa vipengele vya mawasiliano ya kiafya vinavyohusiana na UVIKO-19 katika nyimbo hizo za Kiswahili. Tatu, Matini mbalimbali yenye vipengele vya ugonjwa wa UVIKO-19 yalinukuliwa kutoka kwa nyimbo kisha ujumbe kuchanganuliwa katika matini hayo unaolandana na ugonjwa wa UVIKO-19. Mwisho, usomaji wa kina ulifanywa dhidi ya data zisizo asilia zilizohusiana na UVIKO-19.

### 2.1. Redio katika uhamasishaji wa umma kuhusu UVIKO-19

Redio ni chombo muhimu katika kutekeleza mchakato wa uhamasishaji wa umma. Kwa muda mrefu sasa, watafiti wameonyesha namna vyombo vya habari hasa redio vinatekeleza wajibu mkubwa katika kuwasilisha habari kwa umma na kuihamasisha (Berger na Luckman,1967; Garfinkel,1967 na Goffman,1974). Aghalabu vyombo vya habari huteua kwa makusudi na kuwasilisha habari fulani kwa malengo maalum (Tuchman, 1978).

Redio ni miongoni mwa vyombo vya habari vinavyopendelewa na kutumiwa sana kutokana na ushawishi wake (Drazen, Guenther na Hansen, 2009). Redio imeelezwa kuwa chombo cha habari chenye umuhimu mkubwa sana katika uhamasishaji wa umma kote ilimwenguni (Elliot-Green na wenzake,2016; Seale, 2002). Noar (2006) anadai kuwa ni kutokana na umuhimu wa redio ambapo imekuwa ikitumika kwa muda mrefu katika shughuli ya uhamasishaji wa umma kupitia mawasiliano ya kiafya. Baadhi ya wataalamu wa mawasiliano ya kiafya wanaonelea kuwa redio ndiyo roho ya uhamasishaji wa umma (Day, 2011; Obono, 2011; DeJong, 2010; Kreps & Sivaram, 2009). Vituo vya redio vina jukumu kubwa katika kuongeza ushiriki na kubadilishana maoni, kuboresha na kubadilisha maarifa na ujuzi na katika kukidhi mahitaji ya kiafya na kitamaduni. Pia ina uwezo wa kuwahamasisha watu kwa kujenga juu ya mapokeo ya mdomo kama vile nyimbo ambazo husaidia kufikia mioyo ya watu. Kuna wataalamu wanaohoji kwamba ufanisi wa redio katika uhamasishaji wa umma hupatikana kupitia burudani na elimu (Piotrow & de Fossard, 2003). McCombs & Ghanem (2001) wanadai kuwa namna suala la kiafya linavyofumwa na kuwasilishwa kwenye vyombo vya habari huathiri umma unavyolipokea na kulishughulikia. Kampeni za vyombo vya habari kwa muda mrefu zimekuwa chombo cha kukuza masuala ya afya ya umma hasa matumizi ya redio kama mojawapo ya njia ya kuhamasisha umma dhidi ya magonjwa. Redio inachukuliwa kuwa chombo chenye nguvu katika kuhusisha hadhira iliyolengwa kuhusiana na masuala muhimu ya afya (Brasil & Santos, 2020).

Hivi karibuni, uhamasishaji wa umma kupitia vyombo vya habari umeanza kuwa na ubunifu wa kufuma ujumbe na kuuwasilishwa kwa njia na mitindo mbalimbali. Mojawapo ya njia na mbinu inayoibuka na kupendelewa ni ya uhamasishaji kupitia elimu na burudani kwenye redio. Redio ya kitaifa ya KBC (Kenya Broadcasting corporation), redio Citizen, redio Maisha na redio Jambo ziliimarisha ufahamu dhidi ya janga la UVIKO-19 kwa kufahamisha na kuelimisha wananchi nchini Kenya. Jukwaa la mawasiliano na mitandao ya redio hizi wakati wa mlipuko hadi sasa kuhakikisha umma katika maeneo ya mbali nchini Kenya unapokea taarifa za kuaminika moja kwa moja kutoka kwa wanaafya dhidi ya UVIKO-19. Kwa vile redio inaweza kuwafikia watu kwa urahisi ina athari kubwa katika maisha ya watu. Matangazo ya redio pia ni rahisi kwa wasikilizaji na ni ya mafanikio makubwa ya utangazaji wa redio. Licha ya hayo, redio hizi zinakua mara kwa mara na kuwafikia watazamaji na kuweza kuleta mabadiliko fulani katika maisha ya umma nchini kenya kwa kuwahamasisha dhidi ya masuala mbalimbali ikiwemo UVIKO-19.

## 3. Nyimbo za Kiswahili katika uhamasishaji wa umma kuhusu UVIKO-19 nchini Kenya.

Utafiti ulibaini kuwa nyimbo za Kiswahili zilitumiwa kuhamasisha umma dhidi ya UVIKO-19. Nyimbo nne zilizotumika katika redio ya kitaifa ya KBC (Kenya Broadcasting corporation), redio Citizen, redio Maisha na redio Jambo zilichunguzwa. Nyimbo hizi ni: Wimbo wa Korona, Korona hatari, Corona Virus Song (Wimbo wa Virusi vya korona) na Gonjwa hatari.

### 3.1. Wimbo wa Korona

Wimbo huu unahusu janga la UVIKO-19 na namna lilivyovamia ulimwengu mzima na kuzua simanzi nchini Kenya.Waimbaji wanaeleza kuwa njia iliyofaa dhidi ya janga hili ni kila mmoja kuzingatia maagizo yaliyotolewa na shirika la afya. Wanasema:

> Wakenya kuna ugonjwa wa korona, tunaushauri ulimwengu wote,
> Tunawe mikono kila mara, tufuate maagizo ya afya,
> Tuoshe mikono na sabuni, ziba mdomo ukipiga chafwa,
> Wakati umefika ndugu, tujihadhari na hii korona.
> *Ubeti wa (2), (3) na (7)*

Katika beti hizi, msanii anatoa ushauri kwa umma kuwa ugonjwa huu upo na njia muafaka ya kukabiliana nao ni kunawa mikono kwa sabuni kila mara na kuziba midomo wakati wa kupiga chafya. Anaongezea kuwa ni

vyema iwapo wananchi watatilia mkazo maagizo ya afya yaliyotolewa na wizara husika. Mbali na hayo, anahimiza wananchi kujihadhari na ugonjwa huo wa korona. Kuenea kwa virusi vya UVIKO-19 nchini Kenya kulisababisha maafisa wa umma na wakuu wa vyombo vya habari kuhimiza mara kwa mara unawaji wa mikono kwa sabuni kama njia ya kujilinda dhidi ya UVIKO-19 na magonjwa mengine.

Katika wimbo huu, msanii anaonyesha kuwa iwapo umma itashirikiana, basi wataangamiza "adui" ambaye amewavamia akiwa ni UVIKO-19. Anasema;

Korona ni janga la ulimwengu,
Ni adui asiyeonekana, aaah,
Anahitaji ushirikiano ooh,
*Ubeti (1)*

Kwa mujibu wa kauli hiyo, kundi hili la waimbaji linashauri wananchi wa kenya kuwa na umoja katika juhudi zao za kupigana na "adui" huyo ikilenga UVIKO-19. UVIKO-19 anachukuliwa kuwa adui ambaye ameshambulia umma na ambaye anahitaji umma kushirikiana katika kumkomesha. Ushauri huu unatolewa kwa umma ili watambue kuwa njia bora ya kukabiliana na UVIKO-19 ni serikali kushirikiana na wananchi wote nchini Kenya kwa ajili ya kupambana nao. Katika ubeti wa mwisho msanii anawaarifu wakenya kuwa UVIKO-19 ni ugonjwa hatari kwa kila mtu na hautambui jinsia wala miaka. Anasema:

Korona haijui kasabuni,
Na wala haijui cheochako,
Na wala haijui miaka yako
Uwe mtoto au mzee,
Korona haijui jinsia uwe baba wala mama,

Kulingana na usemi huu, msanii aliwaarifu wananchi kuwa UVIKO-19 ni ugonjwa ambao haubagui miaka wala rika kwa hivyo ni jukumu la kila mmoja kujilinda dhidi yake.

### 3.2. Wimbo wa Korona hatari

Msanii katika wimbo huu anaanza kwa kutoa ujumbe kwa wakenya kuwa wasikilize kwa makini kwa ajili ya maisha yao. Katika wimbo huu, anawatangazia wakenya kuwa UVIKO-19 ni ugonjwa hatari na ni sharti wazingatie masharti yaliyotolewa na serikali pamoja na washikadau husika. Licha ya hayo, anatoa onyo kwa wananchi kuwa ni sharti wajilinde anaposema;

Tusikae karibu, tuwe mbali mita nne,
Salamu tupeane, mikono tusishikane,
Tuvae barakoa, tuzibe pua zetu na midomo
Tuepuke ugonjwa hatari, korona ndugu wakenya.
*Beti za (3) na (10)*

Kauli hii inaonya umma kwamba wasishikane mikono wakati wanaposalimiana, wasikae karibu katika mikutano, wavae barakoa na wazibe pua na midomo yao. Hali hii inaashiria namna ambavyo UVIKO-19 ni hatari na unasababisha vifo iwapo hawatafuata yale yanayostahili. Pia msanii huyu alitoa tangazo kwa wakenya kuwa ugonjwa huu ni hatari na walihitaji kuzingatia masharti ya serikali ili kuyalinda maisha yao dhidi ya UVIKO-19. Anasema:

Tangazo, tangazo nawatangazia wakenya,
Ndugu zetu wakenya korona ni ugonjwa hatari,
Tufuate masharti tuliyopewa na madaktari na tufuate masharti,
*Beti za (2), (7) na (11)*

Kama katika wimbo huu, tafiti za a wataalamu mbalimbali zilionyesha kwamba baada ya Shirika la Afya Duniani kutangaza UVIKO-19 kuwa janga la kiafya, wasanii walijitokeza na kutoa mchango wao kupitia ubunifu wa nyimbo, kuimba na kutumbuiza kwenye mikutano na hata nyimbo zao kutumiwa kwenye redio (Appiah, Walia & Nam, 2022; Aikins, 2020). Watafiti hawa walionyesha namna nyimbo zilitumiwa kukabiliana na janga la UVIKO-19 na kuimarisha afya ya jamii. Hili hufanyika kupitia wasanii kubuni nyimbo zenye ujumbe na maudhui yanayolenga kuigusa jamii, kuihamasisha hadhira na hivyo kujenga msingi wa kuelewa na kuchukua uamuzi.

### 3.3. Corona Virus Song (Wimbo wa Virusi vya korona)

Katika Corona Virus Song kama ulivyotambulika mtandaoni, mwimbaji Sawbow anaonyesha umma kuwa UVIKO-19 ni janga ambalo limewapata na ambalo wanastahili kuwa makini nalo. Anawasihi wakenya kutoa ripoti iwapo wataona dalili zozote kati ya mmoja wao wala wasipuuze namna wengine wamepuuza. Anasema:

Kokohoa, ugumu wa koo kavu,
Joto mwilini, hizi ndizo dalili za korona,
Wenzangu tujichunge
*Ubeti 3*

Katika ubeti huu, mwimbaji anaelimisha umma kuwa, kukohoa na ugumu wa kuwa na koo kavu na kuhisi joto jingi mwilini ni dalili za korona. Aidha, UVIKO-19 ulizua dalili kwa wale walioathirika na iliwabidi wapelekwe karantine. Mtu ambaye alionekana na dalili hizi au mojawapo hakuruhusiwa kutangamana na wengine kabla ya matibabu. Hii inaonyesha kuwa UVIKO-19 haikuwa tu homa ya kawaida namna wengine walidai bali ulikuwa ugonjwa ambao ulizua mabadiliko katika hali ya kiafya ya mwananchi. Mwimbaji anatia umma moyo kuwa uwe na tumaini na kuwa watashinda hali hii, anasema;

Janga hili limetupata, janga kuu la korona,
Nawasihi mjitie moyo, msibabaike tutashinda aah,
Tufuate maagizo ya wizara ya afya,
Tusafishe mikono mara kwa mara,
Tuepuke kukaa kwa vikundi hili jana tutashinda.
*Ubeti wa (1) na (2) na (4)*

Kulingana na kauli hii, mwimbaji anaonyesha kuwa UVIKO-19 ni janga ambalo liliwakumba na kuwatia moyo kuwa wasiwe na hofu bali watashinda. Wimbo huu unawapa tumaini wakenya kwamba iwapo watafuata maagizo ya shirika la afya basi wataibuka kuwa washindi. Unahimiza mabadiliko ya kitabia yatakayozuia maambukizi miongoni mwa umma. Nyimbo kama utanzu wa fasihi huwa na mawazo mazito na hutumiwa kuonyesha uhusiano wa jamii, migogoro, kuliwaza, kuelimisha, kutumbuiza na kuburudisha (Wamitila, 2004). Matumizi ya nyimbo katika jamii ni suala ambalo

limefanyiwa utafiti wa kina kwa muda mrefu (Scialo na wenzake, 2020; McConnell, 2016; na Dillon, 2007). Kwa mfano Scialo na wenzake (2020) wanasema kuwa nyimbo hutumika katika kuleta mabadiliko ya kitabia kwa wanajamii.

### 3.4. Wimbo wa Gonjwa hatari

Msanii maarufu wa wimbo huu ni Matwiga Hesbon. Aliarifu umma kuwa ni vyema kuzingatia yale wanayoambiwa la sivyo wataangamia. Aliongezea kuwa ugonjwa wa UVIKO-19 umewaua watu wengi bila kubagua yeyote. Anakosoa umma na kudai kuwa ugonjwa huu ni hatari kwa wote. Anasema:

Hii ni kwa ajili yako wewe na mimi
Ohh bila hivyo tusipozingatioa yale tunayoambiwa
Tutaangamia na hili gonjwa hatari
*Ubeti wa (1)*

limeua wengi, wenye majina na pesa zao
Ndugu chukua hatari mchezo weka kando
*Ubeti wa (2)*

Ugonjwa hili halibagui mtoto wale mzee, tajiri wala maskini,
Rangi ya mtu hata sura, kiongozi na asiye kiongozi
Asiyezingatia maagizo na asiyejipenda
*Ubeti wa (5)*

Kulingana na kauli hii, mwimbaji anaarifu umma kuwa ugonjwa wa UVIKO-19 ni janga ambalo linaathiri kila mtu. Halichagui hadhi, rangi au hata umri. Kwa mujibu wake, UVIKO-19 ni ugonjwa ambao unaangamiza mtu ambaye haoni manufaa ya kujilinda na kujizuia nao. UVIKO-19 ulikuwa janga ambalo lilienea kila sehemu ya dunia na kusababisha vifo vya mamilioni ya watu wazima na hata kwa vijana na watoto. Ugonjwa huu sugu ulizua taharuki kwa serikali na umma ndiposa wizara ya afya kupitia serikali ikatoa tangazo kwa kila mmoja kupata kufahamu athari zake na kujilinda na familia yake. Matokeo haya yanalingana na maoni ya utafiti wa Thompson, Nutor & Johnson (2021) ambao nilionyesha kuwa nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi zilikuwa na manufaa mno katika kuhamasisha umma wakati wa UVIKO-19. Katika utafiti huu, nyimbo za Kiswahili zilionya, kushauri, kuelimisha na kuarifu kwa minajili ya kuhamasisha umma kuhusu hatari UVIKO-19.

Tafiti za awali zimeripoti jinsi nyimbo ziliweza kutumika kama njia ya elimu na kuongeza ufahamu katika muktadha wa afya ya umma (Bekalu, 2015) Hivyo basi, matumizi ya nyimbo katika kutoa ufahamu, mitazamo na kubadili tabia dhidi ya magonjwa ya kuambukiza kama UVIKO-19 si jambo jipya barani Afrika. Kuhusiana na UKIMWI na Ebola, kwa mfano, utafiti ulionyesha jinsi wasanii maarufu katika kanda iliyojumuisha ujumbe wa kukuza afya na maelezo ya kimsingi kuhusu magonjwa haya na hatua za kuzuia katika nyimbo zao (Frishkopf, 2017; Stone, 2017; Bastein, 2009; Sweat, 2008). Mnamo 2000, kampeni iliyopewa jina la "Acha UKIMWI: Penda maisha" ilihusisha video za nyimbo zilizotayarishwa na wanamuziki kule Ghana ili kuongeza uelewa kuhusu UKIMWI nchini. Kampeni hiyo ilitekelezwa na Chuo Kikuu cha Johns Hopkins na Taasisi ya Masoko ya Jamii ya Ghana. Ililenga kuondoa unyanyapaa wa UKIMWI, kuhimiza utunzaji na kusihi umma kutoa na msaada kwa watu wanaoishi na UKIMWI (Sweat, 2008).

### 3.5. Nyimbo katika Uhamasishaji wa Umma

Utafiti uliofanywa na Thompson, Nutor & Johnson (2020) ulionyesha kuwa nyimbo ziliweza kutumika kuelimisha na kusambaza habari kuhusu majanga ya afya ya umma. Kwa kuzingatia mbinu ya uelimishaji, wanasema kuwa nyimbo zilitumika kuhamasisha watu kuhusu UVIKO-19 nchini Ghana, nchi ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.Nyimbo ni sehemu ya elimu, mkakati maarufu ambayo inaruhusu ujumbe kuhusu elimu kuongezwa kwenye vyombo vya habari vya burudani ili kubadilisha tabia na mitazamo (McConnell,2016).

Katika Makala hii, nyimbo za Kiswahili ziliteuliwa na kuchunguzwa ili kueleza namna zilivyotumiwa kwenye stesheni za redio teule kuhamasisha umma dhidi ya janga la UVIKO-19 nchini Kenya.Makala hii ilijikita kwenye nyimbo za wasanii wa Kiswahili na kutathmini mchango wao katika vita dhidi ya UVIKO-19. Pia, ulizingatia ubunifu wa nyimbo na utumbuizaji unavyojitokeza kama elimu na burudani. Ujumbe kwenye nyimbo za Kiswahili ulichanganuliwa kwa kurejelea vipengele muhimu vinavyochangia uhamasishaji wa umma.

## 4. Hitimisho na Mapendekezo

Makala hii iliangazia nyimbo za Kiswahili kama mkakati wa kuhamasisha umma dhidi ya UVIKO-19 kwenye stesheni ya redio ya KBC (Kenya Broadcasting corporation), redio ya Citizen na redio Maisha. Inaangazia chimbuko la UVIKO-19 nchini Kenya na kuweka bayana bayana namna ambavyo nyimbo za Kiswahili kwenye redio zilikuwa mkakati bora katika kuonya, kushauri na kuelimisha umma dhidi ya UVIKO-19. Inaonyesha manufaa ya nyimbo hizi katika kushauri, kuhimiza umma na kubadili tabia zilizowezesha kukumbana na Korona. Zilielekeza kuhusu mikakati iliyopendekezwa na wizara ya afya; zikashauri kuhusu taarifa za kweli na uvumi na hivyo kutoa mwelekeo mwafaka kwa umma kwa njia ya burudani. Makala hii inahimiza wasanii wa Kiswahili na Lugha asilkia kutumia nyimbo na tanzu nyingine katika kuelimisha umma kuhusu majanga na masuala mengine yanayoathiri jamii. Inapendekeza tafiti zaidi kuhusu matumizi ya tanzu za Fasihi katika kutatua matatizo ya jamii.

## Marejeleo

Abuya, T., Austrian, K., Isaac, A., Kangwana, B., Mbushi, F., Muluve, E.& White, C. (2020). Experiences among adults and adolescents during the COVID-19 pandemic from four locations across Kenya—Study description.

Aikins, A. (2020). 'Colonial virus'? Creative arts and public understanding of COVID-19 in Ghana. Journal of the British Academy, 8, 401-413.

Appiah, B., Walia, B., & Nam, S. H. (2022). Promoting COVID-19 vaccination through music and drama—Lessons from early phase of the pandemic. British Journal of Clinical Pharmacology, 88(2), 437.

Bastien, C. (2009). Spontaneous K-complexes in chronic psychophysiological insomnia. Journal of Psychosomatic Research,

Brasil & Santos, C. F. (2020). Reflections about the impact of the SARS-COV-2/COVID-19 pandemic on mental health. Brazilian journal of psychiatry, 42, 329-329.

Bekalu, M. A., & Eggermont, S. (2015). Aligning HIV/AIDS communication with the oral tradition of Africans: A theory-based content analysis of songs' potential in prevention efforts. Health Communication, 30(5), 441-450.

Berger, P., & Luckmann, T. (1967). TheSocial. Construction Of Reality, New York: Garden City

Brug, J., Aro, A. R., Oenema, A., De Zwart, O., Richardus, J. H., & Bishop, G. D. (2004). SARS risk perception, knowledge, precautions, and information sources, the Netherlands. Emerging infectious diseases, 10(8), 1486.

Day, G. M. (2011). Current approaches to predicting molecular organic crystal structures. Crystallography Reviews, 17(1), 3-52.

DeJong, N. (2010). Social norms marketing campaigns to reduce campus alcohol problems. Health Communication, 7, 615-620. https://doi.org/10.1080/10410236.2010.4968 45

Dillon, M. (2007). Governing through contingency: The security of biopolitical governance. Political geography, 26(1), 41-47.

Drazen, Y., Guenther, L., & Hansen, J. (2009). Public awareness campaigns. Child maltreatment prevention: Toward an evidence-based approach, 17.

Elliott-Green, A., Hyseni, L., Lloyd-Williams, F., Bromley, H., & Capewell, S. (2016). Sugar-sweetened beverages coverage in the British media: An analysis of public health advocacy versus pro-industry messaging. BMJ Open, 6(7).

Fizke, E. (2018). Executive function plays a role in coordinating different perspectives, particularly when one's own perspective is involved. Cognition, 130(3), 315-334.

Frishkopf, M. (2017). Popular music as public health technology: music for global human development and "Giving Voice to Health" in Liberia. Journal of Folklore Research, 54(1-2), 41-86.

Garfinkel, H. (1967). Studies in. Studies in ethnomethodology. Englewood Cliffs, NJ.

Goffman, E. (1974). Frame analysis: An essay on the organization of experience. Northeastern UP.

Jin, X., Lian, J. S., Hu, J. H., Gao, J., Zheng, L., Zhang, Y. M.,& Yang, Y. (2020). Epidemiological, clinical and virological characteristics of 74 cases of coronavirus-infected disease 2019 (COVID-19) with gastrointestinal symptoms. Gut, 69(6), 1002-1009.

Kreps, G., & Sivaram, R. (2009). Strategic healthcommunication across the continuum of breast cancer care in limited resource countries. Cancer Supplements, 113(8), 2331- 337. https://doi.org/10.1002/cncr.23832

Lisco, G., De Tullio, A., Stragapede, A., Solimando, A. G., Albanese, F., Capobianco, M., & Triggiani, V. (2021). COVID-19 and the endocrine system: a comprehensive review on the theme. Journal of clinical medicine, 10(13), 2920.

Mackay, I. M., & Arden, K. E. (2015). MERS coronavirus: diagnostics, epidemiology and transmission. Virology journal, 12, 1-21.

Mahato,C., & Suryavanshi, S. (2020). Knowledge, attitude, and practices towards COVID-19 among nurses, ward attendants, and housekeeping staff at a tertiary psychiatric institute in India. Int J Community Med Public Heal, 7(12), 5035.

Momattin, H., Mohammed, K., Zumla, A., Memish, Z. A., & Al-Tawfiq, J. A. (2013). Therapeutic options for Middle East respiratory syndrome coronavirus (MERS-CoV)–possible lessons from a systematic review of SARS-CoV therapy. International Journal of Infectious Diseases, 17(10), e792-e798.

McCombs, M. E., & Gharen. (2001). The agenda-setting function of mass media. Public opinion quarterly, 36(2), 176-187.

McConnell, A.(2016). Understanding policy responses to COVID-19: The stars haven't fallen from the sky for scholars of public policy. Journal of European Public Policy, 28(8), 1115-1130.

Noar, S. M. (2006). A 10-year retrospective of research in health mass media campaigns: where do we go from here? Journal of health communication, 11(1), 21-42.

Obono, K. (2011). Media strategies of HIV/AIDS Communication for Behavior Change in South West Nigeria, Africana. 8,148-170.

O'Sullivan, P. B. (1983). Bridging the mass-interpersonal divide synthesis scholarship in HCR. Human Communication Research, 25(4), 569-588.

Piotrow, P. T., & De Fossard, E. (2003). Entertainment-education as a public health intervention. In Entertainment-education and social change (pp. 61-82). Routledge.

Rabbani & Mahtab (2020). The Coronavirus Disease 2019 (COVID-19): The Prevalence, Recovery, and Prognosis of Olfactory Dysfunction (OD).

Sadique, M. Z., Edmunds, W. J., Smith, R. D., Meerding, W. J., De Zwart, O., Brug, J., & Beutels, P. (2007). Precautionary behavior in response to perceived threat of pandemic influenza. Emerging infectious diseases, 13(9), 1307.

Sayer, R. (2006). Principles of awareness raising: Information Literacy, a case study. Thailand:Communication and Information(CI) Publishers

Seale, C. (2002). Quality issues in qualitative inquiry. Qualitative social work, 1(1), 97-110.

Scialo, F., Daniele, A., Amato, F., Pastore, L., Matera, M. G., Cazzola, M., & Bianco, A. (2020). ACE2: the major cell entry receptor for SARS-CoV-2. Lung, 198, 867-877.

Shafiq, A., Sindhu, T. N., & Al-Mdallal, Q. M. (2021). On the analysis of number of deaths due to Covid− 19 outbreak data using a new class of distributions. Results in Physics, 21, 103747.

Stone, E. S. I., Umscheid, C. A., Bratzler, D. W., Leas, B., Stone, E. C., Kelz, R. R., ... & Healthcare Infection Control Practices Advisory Committee. (2017). Centers for disease control and prevention guideline for the prevention of surgical site infection, 2017. JAMA surgery, 152(8), 784-791.

Suryavanshi, N., Kadam, A., Dhumal, G., Nimkar, S., Mave, V., Gupta, A., & Gupte, N. (2020). Mental health and quality of life among healthcare professionals during the COVID-19 pandemic in India. Brain and behavior, 10(11), e01837.

Sweat, M. D., O'Reilly, K. R., Schmid, G. P., Kennedy, C. E., & Denison, J. A (2008). HIV voluntary counseling and testing and behavioral risk reduction in developing countries: a meta-analysis, 1990–2005. AIDS and Behavior, 12, 363-373.

Tuchman, G. (1978). Making news: A study in the construction of reality.

Thompson,T and Schulz,P.(2021).Health Communication Theory: John Wiley and Sons Inc publishers

Thompson, R. G., Nutor, J. J., & Johnson, J. K. (2021). Communicating awareness about COVID-19 through songs: An example from Ghana. Frontiers in public health, 8, 607830.

UNEP. Division of Early Warning, & Assessment. (2006). UNEP year book 2006: emerging issues in our global environment. UNEP/Earthprint.

Van der Weerd, W., Timmermans, D. R., Beaujean, D. J., Oudhoff, J., & Van Steenbergen, J. E. (2011). Monitoring the level of government trust, risk perception and intention of the general public to adopt protective measures during the influenza A (H1N1) pandemic in the Netherlands. BMC public health, 11, 1-12.

Wamitila, K.W. (2004). Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi. Nairobi: English Press.

WHO. (2020). Interim case reporting form for 2019 Novel Coronavirus (2019-nCoV) of confirmed and probable cases: WHO minimum data set report form, 21 January 2020 (No. WHO/2019-nCoV/Surveillance_CRF/2020.1). World Health Organization.

WHO. (2023). COVID-19 vaccination in humanitarian settings: action plan from a joint convening and contributions to broader pandemic preparedness. World Health Organization.

Yıldırım, M., & Solmaz, F. (2022). COVID-19 burnout, COVID-19 stress and resilience: Initial psychometric properties of COVID-19 Burnout Scale. Death Studies, 46(3), 524-532.

Zorica, M. B. (2014). Edutainment at the higher education as an element for the learning success. In EDULEARN14 Proceedings (pp. 4089-4097). IATED.